# *BARUA #07; UBATIZO WA MAFANIKIO.*

Karibu rafiki yangu mpendwa kwenye barua yetu ya mwaka wa mafanikio.

Kwenye barua hii tunakwenda kujadili kwa kina dhana muhimu ambayo wengi wamekuwa hawaipi uzito kwenye maisha ya mafanikio.

Dhana hiyo naipa jina la **UBATIZO WA MAFANIKIO**.

Nina hakika unajua maana ya ubatizo, kwa dini za Kikristo ni kitendo cha kuzaliwa upya, kuyaacha maisha ya zamani na kuyaanza maisha mapya.

Ubatizo ni tukio muhimu, linalovunja yale yote ya nyuma na kumfanya mtu azaliwe upya, awe mpya na huru zaidi kuyaishi maisha sahihi kwake.

# Historia ya dhana ya ubatizo.

Dhana hii ya ubatizo imekuwepo tangu enzi na enzi kwenye kila aina ya jamii.

Jamii nyingi zilikuwa na utamaduni wa jando na unyago, ambacho kilikuwa ni kipindi ha vijana kuyaacha maisha ya utoto na kuingia maisha ya utu uzima. Kutoka kuwa chini ya himaya ya wazazi na kwenda kuanzisha himaya zao wenyewe.

Lakini mtu kuondoka kwa wazazi na kwenda kuanza maisha siyo zoezi rahisi, ni maisha mapya kabisa ambayo yana majukumu makubwa. Hivyo kabla mtu hajapewa majukumu hayo, anapewa mafunzo na kujaribiwa kama kweli yuko tayari.

Na hapo ndipo jando na unyago vilikuwa na nafasi ya kuwaandaa watu kwa majukumu makubwa yanayokuja mbele yao.

Kwenye kila jamii, kulingana na changamoto zake, vijana waliandaliwa na kupimwa kama kweli wameiva kwa jukumu la kuanza maisha yao.

Mfano kwa jamii za wafugaji ambapo wanyama wakali ni changamoto kubwa kwao, vijana walipimwa kwa kuweza kumuua mnyama mkali kama Simba. Kama kijana ataweza kumuua mnyama huyo basi anaonesha kwamba anaweza kulinda mji wake na hivyo anayaweza majukumu ya maisha.

Jamii nyingine zilikuwa na mafunzo na mitihani yake ili kuhakikisha wanawaandaa watu sahihi wa kuweza kuyakabili maisha. Na hayo yalifanyika kwa vijana wote, wa kike na wa kiume.

Hili la kuwapika na kuwapima watu kabla hawajapewa majukumu makubwa halikuishia tu kwenye ngazi ya jamii, bali pia lilikuwepo kwenye vikundi na taasisi mbalimbali.

Mfano kwenye taasisi za kielimu, ili mtu aweze kupanda ngazi na kufika ngazi ya uprofesa, lazima awe chini ya maprofesa wengine kwa kipindi kirefu, wamfundishe na kumpima kwa namna mbalimbali kabla hawajajiridhisha kweli anafaa kupewa jukumu kubwa la uprofesa.

Kupitia mifumo hiyo ya mafunzo na kupimwa, ambayo haikuwa rahisi, wale waliopewa majukumu walikuwa tayari kuyakabili na mambo yalikwenda vizuri.

Lakini sasa tunaishi kwenye zama tofauti, zama ambazo mifumo hiyo ya mafunzo na kupimwa inakufa na kukosa nguvu kabisa. Zama ambazo watoto wanalelewa kama malaika, wakiwa vijana wanachukuliwa kama wafalme au malkia. Ni mpaka wanapokuja kuyakabili maisha ndiyo wanagundua kwamba hawakuwa tayari.

Na hili linaonekana wazi kwa namna ambavyo watu wanachelewa kujitegemea, namna ambavyo vijana wenye umri mkubwa na hata elimu kubwa bado wanawategemea wazazi wao kuyaendesha maisha yao kwa sababu hawajapata ajira. Namna ambavyo mtu anaweza kuwa tayari ana maisha yake na familia yake, lakini wazazi wake ndiyo wanamfanyia maamuzi ya maisha yake. Namna ambavyo mtu anakutana na changamoto kwenye maisha yake, badala ya kuitatua

anaikimbia, anakimbilia kwenye ulevi au mitandao ya kijamii.

Haishangazi kwa nini maisha yanakuwa magumu kwa wengi, kwa sababu wengi hawajaandaliwa na kujaribiwa kama kweli wako tayari kwa maisha. Wengi wanaingia kwenye maisha wakiwa hawajapikwa na kupimwa, na maisha yanawanyoosha kisawasawa.

Dhana hii ya maandalizi kwa mabadiliko ya maisha haipo tu kwa binadamu, bali ipo kwa kila kiumbe hai. Kila kiumbe kina mifumo yake ya kuandaa na kupima uwezo na utayari wa kuyakabili maisha na changamoto zake. Na yote hiyo ni kuhakikisha kiumbe anakuwa hai, anapata chakula, anaepuka hatari na kuzaliana.

## Dhana ya ubatizo kwenye mafanikio.

Nimekuwa nasema hivi; siku utakayojiambia tu kwamba unataka kufanikiwa, ndiyo siku hiyo hiyo dunia itaanza kukujaribu kama kweli unamaanisha unachojiambia au unajidanganya tu.

Hivi hujawahi kujiambia unaachana kabisa na pombe, halafu siku hiyo hiyo marafiki zako wanakupigia simu kwamba wanakutana pamoja kuburudika na hawataki kukukosa? Au unakutana na mtu kwa mazungumzo anaanza kutumia kilevi na kukushawishi na wewe utumie, japo kidogo na unapokuja kustuka umeshalewa?

Huenda pia umewahi kujiambia hutaki tena kuchepuka au kuwa na mahusiano mengi, ukakaa chini na kuangalia mahusiano yote ambayo umekuwa nayo na kuamua yapi unaachana nayo kabisa na kubaki kwenye mahusiano makuu. Hata siku haiishi katika mahusiano uliyovunja unaanza kutafutwa na kushawishika kurudi ulikojaribu kuondoka?

Inaweza kuwa pia umejiwekea mkakati kwamba unataka kufanya kwa ubora wa hali ya juu kabisa kazi zako kwa pale ulipoajiriwa, unataka kutoa thamani kubwa kwa sababu umejifunza kwamba kazi unayoifanya ni yako na siyo ya bosi wako. Lakini unapoanza siku ya kwanza wafanyakazi wenzako wote wanakushangaa,

wanakuambia acha kiherehere, hakuna anayejali unachofanya. Unapojaribu kuendelea hivyo wanaanza kukutengenezea majungu na hatimaye unaona bora usijisumbue.

Au unaweza kujiambia unaanza kuweka akiba, kwa sababu umekuwa huna nidhamu ya fedha na hilo limekuwa kikwazo kwako, unatumia kipato chote na kikiisha unakopa. Hujawahi kuwa na kiasi kikubwa cha fedha, kwani unapokea na kulipa madeni. Siku umeanza kuweka akiba na inakuakua kiasi yanaanza kutokea mambo yanayopelekea utumie akiba ile.

Umejifunza umuhimu wa kuacha kukimbizana na fursa mpya kila siku, uchague kitu kimoja na uweke juhudi na muda, unachagua kweli, lakini siku chache baadaye unasikia kuna fursa mpya imekuja, fursa ambayo hupaswi kuikosa, unawaona kabisa wengine wakinufaika na kuona hakuna ubaya na wewe kujaribu, unaingia na mambo yanaishia kuwa yale yale, hunufaiki kama ulivyodhani na zaidi unakuwa umepoteza muda, nguvu na hata fedha.

Naweza kuendelea kukupa mifano mingi, ambayo inamtokea kila mmoja wetu. Mifano hiyo inaonesha jinsi gani dunia haiwezi kukupa kitu chochote kile kirahisi, lazima ikupime kwanza kama kweli upo tayari kwa kitu hicho.

Ni kwenye kipimo hicho cha dunia ndipo wengi wanaposhindwa na ndiyo maana licha ya wengi kupambana, ni wachache mno wanaoanikiwa.

Kuna sifa na tabia nyingi zinazowatofautisha waliofanikiwa na walioshindwa, lakini kuna kitu kimoja ambacho kimekuwa hakizungumziwi sana, kitu hicho ndiyo tunajifunza leo; UBATIZO WA MAFANIKIO.

Wale wanaofanikiwa wanakuwa wameupata ubatizo wa mafanikio, wanakuwa wamepitia mchakato mgumu wa kupikwa na kupimwa, wanakuwa wamelipa gharama kubwa kiasi kwamba hawapo tayari kuishia njiani. Dunia inapokutana na watu hawa, inasalimu amri na kuwapa wanachotaka, kwa sababu hakuna namna watakata tamaa.

Wale wanaoshindwa wanakuwa hawajapata ubatizo wa mafanikio. Wanakuwa wanayataka kweli mafanikio, lakini hawajapikwa na kupimwa, hawajaumia na kulipa gharama kubwa kiasi cha kuendelea na mapambano. Hawa wanapokutana na ugumu wowote hukimbilia kuacha na kwenda kuanza kitu kingine.

Muda, nguvu na gharama ambazo wanatumia waliofanikiwa na walishindwa zinafanana na kulingana, lakini matokeo yao ni tofauti kabisa, na hayo yanatokana na kama mtu amepata ubatizo au la.

## Ubatizo wa mafanikio ni nini?

Ubatizo wa mafanikio ni kuzaliwa upya, ni kufanyika kuwa mtu mpya ambaye mafanikio lazima yaje kwako.

Ni kubadilika kabisa vile ulivyo na yale unayofanya kwa namna ambayo hurudishwi nyuma au kukwamishwa na kitu chochote.

Ni agano unalokuwa umeweka na maisha yako, kwamba kuna matokeo mawili tu kwenye

maisha yako, KUPATA UNACHOTAKA au KUFA UKUWA UNAPAMBANA KUPATA UNACHOTAKA. Hakuna njia nyingine nje ya hizo.

Ubatizo wa mafanikio ni kuwa na ujasiri wa kuishi na kusimamia kile sahihi na kinachokufikisha kwenye mafanikio yako, bila ya kujali wengine wanasema au kufanya nini.

Ni kuchagua kuyaishi maisha ya mafanikio, kwa sababu ndiyo maisha pekee unayoweza kuishi na hakuna namna nyingine unayoiona ikifaa kuyaendesha maisha yako.

Ubatizo wa mafanikio ni gharama unayoilipa, kafara unayoitoa kiasi kwamba huwezi kurudi tena nyuma, huwezi tena kufanya kilicho tofauti na unachotaka.

Na muhimu zaidi, ubatizo wa mafanikio ni kuwa tayari kupokea jukumu la mafanikio, kuwa tayari kuyatuliza mafanikio yanapokuja kwako, kwa kuyatumia vizuri na kuleta manufaa kwako na kwa wengine.

## Hasara ya kukosa ubatizo wa mafanikio.

Kama umesoma kwa umakini hapo maana ya ubatizo wa mafanikio, utakuwa umeshaona wazi hasara za kukosa ubatizo huo kwenye maisha yako mwenyewe.

Utakuwa umeona ni jinsi gani kwa miaka mingi umekuwa unahangaika kufanikiwa, lakini ukikutana na ugumu unaacha na kwenda kuanza kitu kingine, siku unakuja kukutana na mtu amefanikiwa kwenye kile kile ulichoacha na kujilaumu kwa nini uliacha.

Utakuwa umeona kwa nini baadhi ya watu wanapata mafanikio kidogo na kuanguka vibaya, kwa sababu wanakuwa hawajajiandaa kupokea jukumu la mafanikio. Mtu anaanzia chini, anapambana kweli na kuyapata mafanikio, lakini baada ya hapo anaanza kufanya starehe, anatapanya fedha na mali na hilo linampelekea kuanguka vibaya. Na wengi wanapoanguka hawawezi kuinuka tena.

Kukosa mafanikio na kupata mafanikio lakini kuyapoteza ndiyo hasara kubwa mbili za kukosa ubatizo wa mafanikio.

## Unapataje ubatizo wa mafanikio?

Baada ya kuona umuhimu wa ubatizo kwenye mafanikio, sasa tujifunze jinsi ya kupata ubatizo wa mafanikio, lakini kabla ya hilo, tuone jinsi imani za kishirikina zinawasaidia watu kufanikiwa.

### Kafara na masharti.

Kuna watu wamekuwa wanaamini kwenye imani za kishirikina ili kupata mafanikio ya utajiri na mali. Na wale wanaoamini kwenye hayo, kweli wanaonekana kupata utajiri huo. Lakini wengi baadaye hushindwa kudumu kwenye utajiri wa aina hiyo na kupoteza kila kitu kwa sababu wanakuwa hawajui msingi sahihi uliowapa utajiri ni nini.

Ushirikina, majini na imani nyingine za aina hiyo zinazowapa watu utajiri na mali, zinafanya kazi kwa dhana ya ubatizo.

Mtu anapoingia kwenye imani hizo anapitia ubatizo mkali sana, anapokea maagano ambayo yanamfanya awe na nidhamu kali inayomfanya afanikiwe.

Wale wanaoingia kwenye imani hizo huwa wanapitishwa kwenye mambo mawili;

Jambo la kwanza ni kutoa kafara, wanaambiwa watoe kile wanachokipenda sana, iwe ni kitu au mtu, kile wanachokipenda kuliko vyote basi wanapaswa kukipoteza. Hii ni hatua ya kwanza ya ubatizo ambayo inamfanya mtu alipe gharama kubwa. Kwa kulipa gharama hiyo, mtu hawezi tena kurudi nyuma. Kama umekuwa tayari kupoteza kile unachokipenda kuliko vyote kwenye maisha yako ili kupata kitu fulani, basi lazima utakithamini mno kitu hicho, hutakata tamaa kwa namna yoyote ile.

Jambo la pili ni masharti makali, hapa mtu anapewa masharti makali mno ambayo anapaswa kuyafuata bila ya kuleta sababu yoyote ile. Na kama asipofuata masharti hayo, basi atapoteza kila alichopata. Masharti

yanaweza hata yasiwe na maana yoyote, lakini ni masharti yanayomfanya mtu awe na nidhamu ya hali ya juu mno, kwa sababu anahofia kupoteza kila alichopata.

Sasa rafiki yangu, hebu pata picha tu, wewe A na mwenzako B mmeingia kwenye biashara ya aina moja. Wewe umeingia kwa sababu umesikia watu wanasema inalipa na unataka ufanikiwe. Ila mwenzako B ametoa kafara ya kile anachopenda sana na amepewa masharti makali kwamba kila siku saa kumi na mbili kamili imkute ameshafika eneo la biashara ajifungie huko ndani mpaka saa moja kamili ndiyo afungue biashara yake, siku atakayoacha kufanya hivyo biashara itakufa kabisa.

Sasa wewe niambie tu, nani ana nafasi kubwa ya kufanikiwa kwenye biashara kati yako wewe na huyo mwenzako. Wakati wewe unaamka ukiwa umechoka na kujiambia leo utachelewa kufungua, mwenzako hajali amechoka au la, saa kumi na mbili lazima imkute kwenye eneo la biashara na saa moja lazima afungue, ni lazima,

siyo kujisikia na kama hatafanya hivyo basi atapoteza kila kitu.

Unaweza kuona ni jinsi gani imani hizo zinaweza kumsukuma mtu kufanikiwa mno. Lakini kama nilivyoeleza pia huwa zinawaangusha wengi, kwa sababu hawajui msingi ulio nyuma ya imani hizo, ambacho ndiyo tunajifunza kwa kina hapa.

## Inabidi ujibatize mwenyewe.

Kitu kikubwa ambacho jamii inakosa ni mfumo sahihi wa kuwabatiza watu kuhusu mafanikio. Na hiyo ni kwa sababu asilimia zaidi ya 90 ya watu kwenye jamii hawana mafanikio makubwa. Na hata wale ambao wana mafanikio makubwa wamekuwa wanaonekana ni watu wabaya na wanaowanyonya wengine. Hivyo wamekuwa wanajificha na mafanikio yao, hawathubutu hata kuyazungumzia.

Hilo linafanya jamii ikose watu wa kuwabatiza wengine kuyafikia mafanikio na hapo jukumu linabaki kuwa lako mwenyewe.

Kama unataka kuyafikia mafanikio makubwa, basi ni lazima ujibatize wewe mwenyewe. Lazima ujijengee maagano ambayo utayaishi na kuyasimamia kila wakati, bila ya kujali nini kinaendelea na wengine wanasema au kufanya nini.

Na mchakato wa kujibatiza mwenyewe unapotia hatua mbili tulizojifunza hapo juu; KAFARA NA MASHARTI.

## Mchakato wa kujibatiza mwenyewe.

Tayari unajua nini unataka kwenye maisha yako, una ndoto na maono makubwa ambayo unataka kuyafikia. Kikwazo kikubwa kinachoweza kuwa kinakukabili sasa ni kukosa ubatizo. Na hapa tunakwenda kujifunza ubatizo wa mafanikio, ambao utaufanya leo na kuishi maagano unayojiwekea leo kwenye kila siku ya maisha yako.

# Toa kafara (zaliwa upya).

Msingi wa kwanza kwenye ubatizo wa mafanikio ni kutoa kafara, kwa kuwa tayari kupoteza kile ambacho unakipenda sana.

Usiogope, hapa sikuambii uwaue wazazi wako, wala sikuambii umuue mtoto wako unayempenda sana, au uchinje ng'ombe.

Sitaki ubebe dhambi au damu za wengine, bali nakuambia ubebe dhambi yako wewe mwenyewe.

Kafara pekee unayopaswa kuitoa kama unataka kufikia mafanikio makubwa, ni wewe mwenyewe.

Ndiyo, kama unataka kufikia mafanikio makubwa unayotaka, lazima ujiue wewe mwenyewe na uzaliwe upya, lazima uyafute maisha yako yote ya nyuma na kuanza maisha mapya sasa.

Iko hivi rafiki, kitu pekee ambacho kimekuwa kikwazo kwako mpaka hapo ulipofika, ni wewe mwenyewe.

Kitu pekee kinachokuzuia usipate mafanikio makubwa, ni mafanikio kidogo uliyonayo.

Kitu pekee kinachofanya usipate kazi inayolipa zaidi au biashara yenye faida kubwa, ni kazi au biashara inayokulipa kidogo sasa.

Kumbuka kama unataka kupata kitu ambacho hujawahi kukipata, lazima uwe mtu ambaye hujawahi kuwa.

Na huwezi kuila pipi yako halafu ukabaki nayo, lazima upoteze kizuri ulichonacho ili kupata kilicho bora zaidi.

Hivyo hatua ya kwanza kabisa kwenye ubatizo wa mafanikio ni kujitoa kafara, kulipa gharama kubwa ya kupoteza vile ulivyonavyo sasa na ambavyo ni kikwazo kwako. Utajifunza hapa jinsi ya kufanya hivyo.

## Tatizo ni huyo ng'ombe.

Unakumbuka miaka ya nyuma nimewahi kuandika makala kuhusu ng'ombe aliyekonda, ilikuwa ni mwaka 2017 na makala ilikuwa na kichwa; **Tatizo Lako Ni Huyo Ng'ombe**

**Aliyekonda Ambaye Umeweka Matumaini Yako Yote Kwake.** Kwa wale ambao hawakupata nafasi ya kusoma makala hiyo nitaweka hapa hadithi ya makala ile kwa sababu inahusiana mno na kafara unayopaswa kwenda kuitoa kwenye maisha yako.

*Miaka 3,000 iliyopita, mkulima mmoja masikini aliyeitwa Adir aliishi na mke wake pamoja na watoto watatu, kwenye kijiji kidogo kilichokuwa umbali wa maili 59 kutoka mji wa Yerusalemu. Alikuwa ni mkulima mdogo, aliyefanya kazi kwa juhudi kubwa, lakini bado hakuweza kuwa na uhakika wa kuilisha familia yake.*

*Majirani zake Adir walikuwa masikini pia, japokuwa walimwonea wivu Adir kwa sababu alikuwa na kitu ambacho wao hawakuwa nacho, kitu hicho kilikuwa ni ng'ombe. Ng'ombe huyo hakuwa mkubwa kama tunaowajua sasa, alikuwa ni ng'ombe aliyekondeana sana. Lakini maziwa kidogo ambayo Adir aliweza kupata kutoka kwa ng'ombe huyo, yalimwezesha kupata mahitaji kidogo ya familia yake. Alishukuru sana kwa kuwa na ng'ombe huyo,*

*na hakuwahi kufikiria kumuuza wala kumchinja, kwa sababu maisha yake yalitegemea kwenye ng'ombe yule.*

*Siku moja, kiongozi maarufu wa kiroho alitembelea kijiji alichokuwa anaishi Adir, akiwa na kikundi cha wafuasi wake. Kiongozi huyo alijulikana kama Ba'al Shem Tov. Adir alikuwa mtu wa kiroho, hivyo alifurahishwa sana na ujio wa kiongozi huyo wa kiroho kijijini kwao.*

*Alifurahishwa zaidi pale kiongozi huyo alipopita nyumbani kwake, lakini alishangazwa pale Ba'al aliposema yeye na wafuasi wake wamechoka, hivyo wangefurahi kama wangeweza kupumzika nyumbani kwake. Alipata huzuniko haraka, angewaweka wapi watu wote hao wakati yeye ni masikini mwenye nyumba ndogo tu.*

*Kabla hata hajatoa majibu, Ba'al akawa ameshaingia ndani.*

*Kitu kilichomuumiza Adir zaidi, ni pale kiongozi huyo alipouliza chakula gani kipo. Hapo Adir aliumia kichwa kwa sababu chakula cha familia*

*yake tu ni shida, sasa itakuwaje kwa kuwalisha wanaume tisa? Alimwita mke wake washauriane, akitoa wazo la kumchinja ng'ombe wao. Mkewe akawa anakataa, akimwambia kama ng'ombe huyo ataondoka, maisha hayawezi kwenda tena. Lakini mwisho wa siku, hawakuwa na namna bali kumchinja yule ng'ombe.*

*Adir alijipa moyo kwamba, wakimchinja ng'ombe yule, wageni wangekula na wangebaki na nyama ya kuendelea kula siku mbili tatu. Lakini matumaini hayo yalizimika baada ya chakula kupewa wageni, kila nyama ililiwa na ilibaki mifupa pekee. Hakukuachwa chochote.*

*Baada ya kumaliza kula, Ba'al alimpa taarifa Adir kwamba ameahirisha kupumzika pale, kwa sababu baada ya kula amepata nguvu na hivyo wataendelea na safari, baada ya kusema hayo, waliondoka mara moja. Kichwa cha Adir hakikuweza kutulia, mambo hayo yalitokea haraka sana, akiwa haelewi maisha yataendaje baada ya pale. Kwa kushindwa kutuliza mawazo yake, aliona bora aondoke nyumbani*

*na kwenda msitu wa karibu apunguze mawazo yake.*

*Wakati anakatiza katikati ya miti, akififikiria familia itaendaje baada ya pale, huku ng'ombe aliyekuwa tegemeo akiwa hayupo tena, alisikia sauti mbele yake.*

*Aliposogelea ile sauti, alikuta ni mzee ameanguka na hawezi kuinuka. Kutokana na kuwa mtu wa imani, aliona ni wajibu wake kumsaidia mtu yule. Alienda kwenye mfereji uliokuwa karibu akaja na maji kwa ajili ya mzee yule kunywa. Wakiwa wamekaa pale walianza mazungumzo, kama ilivyo kawaida, walianza kwa kuambiana majina. Adir aliposikia jina la yule mzee, Mordekai, aligundua ni mtu ambaye alishamsikia. Alikuwa ndiye mtu tajiri sana kwenye ukanda mzima waliokuwa wanaishi. Alimuuliza iwapo ni kweli hadithi alizokuwa akisikia kwamba anaishi kwenye jumba la kifahari akiwa na wasaidizi wengi. Alimwambia ndiyo. Alimwambia ana bahati sana, Mzee yule akamwambia siyo kweli, kwa sababu pamoja na mali nyingi alizonazo, bado familia yake*

*ilijali kuhusu fedha zake tu. Walikuwa wanasubiria afe ili wagawane mali zile. Akamwambia huenda watafurahi sana wakijua amefia huko porini. Adir aliyatafakari maisha yake na familia yake pamoja na majirani zake.*

*Pamoja na kwamba hawakuwa na mali, lakini waliishi maisha ya kujali kwa kila mmoja.*

*Adir alikazana kumsaidia mzee yule, wakafika eneo la jirani ambapo walipata punda na kuweza kumbeba mpaka mjini ambapo mzee yule alikuwa rahisi kufika nyumbani kwake. Wakati wanaagana, Mordekai alimwaga Adir akimwambia kwenye maisha yake, yeye ni mtu wa kwanza kumsaidia bila ya kujali fedha zake. Alimwambia hatomsahau kwenye maisha yake.*

*Miaka mitatu baada ya nabii yule Ba' Al Shem Tov kupita kwenye kijiji cha Adir, alirudi tena akiwa na wafuasi wake, safari hii wakiwa wengi zaidi. Walipofika nyumbani kwa Adir walishangaa kuona maisha yake yamebadilika, akiwa na mali nyingi huku maisha yake yakiwa mazuri sana.*

*Wale wafuasi waliomjua miaka mitatu iliyopita, walishangazwa sana, wakimwuliza Adir nini kimetokea mpaka maisha yake kubadilika. Adir aliwaambia kwamba maisha yake yalibadilika baada ya Mordekai kufariki, aliacha sehemu kubwa ya mali zake kwa mtu pekee aliyemsaidia asife. Na mtu huyo alikuwa ni yeye.*

*Ba' Al hakuonekana kusema mengi bali aliishia kutabasamu. Baada ya kuondoka, wafuasi wake walimuuliza kwa nini anatabasamu na kwa nini siku ile walipopita kwa Adir alifanya alivyofanya. Kwa sababu wafuasi wake hawakuwahi kumwona akila nyama nyingi kiasi kile, na wala hajawahi kuvunja ahadi yake. Lakini siku ile alikula kuhakikisha anamaliza na alipomaliza aliahirisha kulala na wakaondoka.*

*Walimwuliza kwa nini alikosa huruma kiasi kile kwa masikini?*

*Na yeye aliwajibu, Adir hakuwa masikini, bali kilichokuwa kinamzuia kuwa na maisha mazuri ni yule ng'ombe aliyekuwa amekonda, hivyo*

*aliamua kuhakikisha ng'ombe huyo anaondoka ili wafikirie tofauti.*

*Yule ng'ombe aliyekuwa amekonda ndiyo kitu pekee alichokuwa anakifikiria, akiwa na matatizo anaangalia pale. Alichukulia maisha yake yote yanategemea kwenye ng'ombe yule, hivyo alipoondoka, ilimbidi afikiri tofauti na hapo ndipo alipokutana na fursa mpya. Isingekuwa kuondoka kwa ng'ombe, angeendelea kumfikiria ng'ombe yule kama kitu pekee cha kuendesha maisha yake.*

Hadithi hii imetupa funzo kubwa mno, kwamba kinachotuzuia tusifike kule tunakotaka kufika, ni kile ambacho tunacho sasa, na hicho ndiyo unachokwenda kutoa kafara ili ufanikiwe.

Swali muhimu la kujiuliza hapa na kuchukua hatua ni ng'ombe gani anayekuzuia sasa? Na hapa unapaswa kujibu kwa maeneo haya matano muhimu ya maisha yako.

## Toa kafara kiakili.

Akili yako ndiyo inayofanya maamuzi yote ya maisha yako, fikra zinazotawala akili yako ndizo

zinazochochea aina ya maamuzi unayofanya na ndiyo zinaamua maisha unayokuwa nayo.

Fikra unazokuwa nazo zinachochewa na kile unachoruhusu kiingie kwenye akili yako, kupitia kusoma, kusikiliza na kuangalia.

Hivyo katika ubatizo wako wa mafanikio unapaswa kuanza kutoa kafara ya kiakili, kwa kujua fikra ambazo zimekufikisha hapo ulipo sasa na kuzivunja kabisa.

Kuhakikisha unaondokana na kila aina ya fikra zinazokuwekea ukomo kwenye kufikia mafanikio makubwa kwenye maisha yako.

Na muhimu zaidi, hakikisha unafuta kabisa fikra hasi kwenye akili yako, acha kuangalia mabaya pekee na kwa kila linalotokea usiangalie kwa upande hasi, badala yake angalia upande chanya.

Chuja kila kinachoingia kwenye akili yako, usiruhusu maarifa na taarifa hasi kuingia kwenye akili yako kupitia kusoma, kusikiliza au kuangalia.

Epuka sana habari na mambo mengine hasi, hayo yanakufanya uone mafanikio hayawezekani na ukate tamaa.

Kuwa chanya na mwenye kuamini mambo yanawezekana mpaka kila mtu akushangae. Maana nguvu ile ile utakayotumia kuwa hasi ndiyo utakayotumia kuwa chanya ila kwenye chanya kuna manufaa kuliko kwenye hasi.

## Toa kafara kiroho.

Kafara nyingine ya kutoa ili ubatizo wako wa mafanikio ukamilike ni ya kiroho. Kuna mambo unayoyaamini kwenye maisha yako ambayo ni kikwazo kwako kufanikiwa.

Kwanza kabisa ni imani kwako binafsi, kama hujiamini, kama huamini unaweza kufanya makubwa na kufanikiwa, kama huamini unaweza kuwa vile unavyotaka, tayari umeshindwa kabla hata hujaanza.

Wale wote waliofanikiwa sana walikuwa wanajiamini kupita kiasi, walijiamini kiasi cha wengine kufikiri labda wana matatizo ya akili.

Hata pale palipoonekana hakuna njia kabisa, wao waliamini njia itajitokeza.

Jijengee imani ya aina hii, jiamini mno, usijitilie shaka hata kidogo, hata pale wengine wanapokata tamaa na wewe na kukuambia huwezi, wewe endelea kujiamini na endelea kuchukua hatua sahihi na utafanikiwa.

Eneo la pili ni kuamini kwenye misingi sahihi, kitu ambacho kitakupa msimamo kwenye kile unachofanya. Bila ya kuwa na misingi unayoiamini na kuisimamia, utayumbishwa na kila mtu na hutaweza kufanikiwa.

Eneo la tatu ni kuamini kwenye mchakato. Usiwe mtu wa kuyumbishwa na matokeo, wewe pambana na mchakato. Unachohitaji ni kuwa kwenye mchakato sahihi na kuendelea nao, mengine yatajipanga yenyewe. Kama unachukua hatua sahihi, matokeo ni swala la muda tu.

## Toa kafara kimwili.

Mwili wako unaupenda sana, umekuwa unauendekeza na kuupa kila unachotaka na hilo limekuwa kikwazo kwako.

Kuna sababu kubwa kwa nini watu wa kiroho huwa wanafunga mara kwa mara, hasa wanapokuwa wanataka kufanya maombi makubwa. Kufunga ni moja ya njia za kuupa mwili nidhamu, ili usiwe kikwazo kwa kile ambacho mtu anataka kukifanya kwa uhakika.

Unapaswa kuutoa mwili wako kafara, uache kuwa unakuendesha na wewe ndiyo uuendeshe.

Hatua ya kwanza kuchukua ni kuchagua vitu gani unalisha mwili wako. Safari ya mafanikio siyo rahisi na ukiwa na afya ambayo ni mbovu, ndiyo unaifanya isiwezekane kabisa. Hivyo kujali mwili wako ni kipaumbele cha kwanza kwako na ulaji sahihi ni muhimu kwako. Epuka sumu zote, kuanzia vilevi mbalimbali, sukari, wanga na vyakula vingine ambavyo ukitumia mwili wako unadhurika.

Hatua ya pili kuchukua kwenye mwili ni kufanya mazoezi, kama shughuli zako ni za kukaa siku nzima au kuwa na mizunguko midogo, unahitaji kufanya mazoezi. Mazoezi yana manufaa mengi kwa mwili, ikiwepo kujenga kinga ya mwili, kukupa nguvu na hamasa ya kufanya kazi zako vizuri na kupunguza uzito pamoja na baadhi ya sumu mwilini.

Hatua ya tatu kwenye kutoa kafara ya kimwili ni kutenga muda wa kupumzika. Mwili wako ni kama betri ya simu, ukiweka chaji unaweza kutumia simu, ila chaji ikiisha huwezi kutumia tena mpaka uweke chaji. Kupumzika ni njia ya kuchaji mwili wako, kuupa nguvu ya kukuwezesha kutekeleza majukumu yako na kukufikisha kwenye mafanikio makubwa.

Unaweza kujiuliza, kula vizuri, kufanya mazoezi na kupumzika si ni mambo ya kawaida kufanya, iweje yawe ni kujitoa kafara? Na nitakujibu ili uwe na mafanikio makubwa, lazima uyafanye kwa namna ambayo wengine hawapo tayari kufanya, namna ambayo wewe mwenyewe

hupendi, lakini huna namna, inakubidi tu usifanye.

Chagua leo nini utalisha na hutalisha mwili wako, mazoezi gani utafanya na muda wa kupumzika kisha fuata mpango huo, siyo kwa kujisikia, kwa sababu ndiyo kafara uliyotoa na ukienda kinyume unaanguka kabisa.

## Toa kafara kwenye mahusiano.

Ulivyo wewe ni wastani wa watu watano wanaokuzunguka, ambao unatumia muda mwingi kuwa nao.

Wanaweza kuwa ndugu wa karibu, marafiki, watu unaofanya kazi au wafanyabiashara wenzako.

Sisi binadamu ni viumbe wa kijamii, huwa tunaathiriwa sana na wale wanaotuzunguka.

Huwezi kufanikiwa kuwazidi wale wanaokuzunguka, ambao unakaa nao kwa muda mrefu, hata uwe na kiu ya mafanikio kiasi gani, watu hao wana nguvu ya kukurudisha ubaki kwenye ngazi zao.

Hivyo hapa unahitaji kutoa kafara ya baadhi ya mahusiano uliyonayo kwenye maisha yako.

Orodhesha watu wote ambao huwa unatumia nao muda wako mwingi, wale ambao mnaongea na kushauriana kila mara.

Kisha kwa kila mtu angalia ametoka wapi, yuko wapi na anaenda wapi. Kwa wale wote ambao hawajapiga hatua kubwa na wameshakata tamaa, kwa maana kwamba hawapambani kufika mbali zaidi, waondoe kwenye ukaribu ulionao.

Huhitaji kuwaambia kwamba mimi na wewe basi, punguza kabisa muda unaotumia na watu hao. Tafuta watu sahihi wa kukuzunguka, wale ambao wamefanikiwa sana au wanaoelekea kwenye mafanikio, ambao mnazungumza lugha moja.

Kama huna watu wa aina hiyo kwenye maisha yako, soma vitabu, wachague watu waliofanikiwa sana huko nyuma na watumie hao kama mamenta wako, soma vitabu vyao, soma mambo yanayowahusu na kila

unachofanya, jiulize kama wangekuwa wao wangefanyaje, hapo utajifunza kufanya kwa ubora zaidi.

Mahusiano yako ya kindugu, kikazi, kibiashara na mengine yanaendekea kama kawaida, ila yale ya karibu mno, wale ambao unawashirikisha mambo yako, unaowaomba ushauri wanapaswa kubadilika. Kwa sababu hakuna mtu anaweza kukushauri kuwa kitu ambacho yeye hajawahi kuwa au hana ndoto za kuwa kitu hicho.

## Toa kafara kwenye kazi/biashara.

Matokeo unayopata kwenye kazi au biashara yako sasa, yametengenezwa na jinsi ambavyo umekuwa unaifanya huko nyuma.

Hivyo kama utaendelea kufanya leo kazi au biashara yako kwa jinsi ulivyofanya jana, kesho usishangae kuendelea kupata matokeo unayopata leo.

Kama unataka kupata matokeo ya tofauti, kama unataka kipato zaidi, kama unataka kubobea

zaidi, kama unataka kukua zaidi kwenye kile unachofanya, anza kufanya tofauti.

Kwanza anza kufikiri tofauti, usiendelee kuichukulia kazi au biashara yako kwa namna unavyoichukulia sasa, kwa kuona ni kitu kidogo na kisicho na uwezo wa kufikia makubwa. Anza kuheshimu kazi na biashara yako, ona hilo ndilo daraja lako la kufikia mafanikio makubwa, hata kama siyo unachotegemea kufanya maisha yako yote.

Pili amini kwenye kile unachofanya, amini kinaweza kukufikisha kwenye mafanikio makubwa na amini unakiweza. Ondoa kabisa imani za kutokuwezekana au kushindwa. Hata kama wengine wanasema ni ngumu au haiwezi kukufikisha mbali, usiamini kama wao, wewe amini kwenye uwezekano na chukua hatua kwa vile unavyoamini.

Kafara kubwa kabisa unayopaswa kuitoa kwenye kazi na/au biashara yako ni mambo unayofanya. Kuna mambo rahisi kufanya na ambayo yanafanywa na kila mtu na kuna

mambo magumu ambayo wengi wanakimbia kuyafanya. Sasa wewe achana na yaliyo rahisi na fanya magumu, tatua matatizo yanayowasumbua wengi na wapo tayari kulipa ili kupata utatuzi.

Kila kazi au biashara ina tatizo gumu ndani yake, ambalo wengi hulikwepa, wewe lijue hili na weka akili, muda na jitihada zako katika kutatua hilo. Ukifanya hivyo kwa kuzingatia yale yote unayojifunza, utaweza kufikia mafanikio makubwa sana kwenye maisha yako.

Hiyo ni hatua ya kwanza kwenye ubatizo wa mafanikio, kutoa kafara maisha yako kwa kuzaliwa upya kwenye maeneo hayo matano.

## Jiwekee masharti.

Sehemu ya pili ya ubatizo wa mafanikio ni kujiwekea masharti.

Kama tulivyoona kwenye ule mfano wa imani za kishirikina, kwamba mtu anapewa masharti ambayo anajazwa hofu kubwa kwamba akiyavunja basi mafanikio yote yanapotea.

Sasa kwenye ubatizo wako unahitaji kujiwekea masharti makali, masharti ambayo yatakujengea nidhamu ya kuchukua hatua kila siku ili kufika kwenye mafanikio makubwa unayoyataka.

Hapa kwenye masharti unapaswa kujua wajibu mkuu ambao wewe unapaswa kuutekeleza ili kufika kwenye mafanikio yako, kisha kujiwekea utaratibu wa jinsi utakavyokuwa unakifanya na kufuata utaratibu huo bila ya kuuvunja, hata iweje.

Hapa unajipangia yale muhimu utakayoyafanya na kuyafanya iwe jua linawaka au mvua inanyesha. Yaani kufanya hayo hakuzuiwi na sababu yoyote ile, unafanya, hilo ndiyo sharti kuu la ubatizo wako wa mafanikio, ili uweze kufika kwenye mafanikio makubwa unayoyataka.

Kukuonesha kwa mfano jinsi ya kujiwekea masharti na nguvu yake, tutaangalia mifano mitatu.

## Musk; likizo itakuua.

Elon Musk, ambaye Januari 2021 ametajwa kuwa mtu tajiri zaidi duniani amejiwekea sharti moja kwenye maisha yake, kwamba kuchukua likizo ni kubaya na kitu chenye laana.

Alifikia sharti hilo baada ya kujaribu kuchukua likizo kwenye kazi mara tatu, na mara zote hazikuwa na matokeo mazuri kwako.

Mara ya kwanza ilikuwa mwaka 2000 ambapo alichukua likizo ya fungate na mke wake na akiwa likizo aliondolewa kwenye ukurugenzi mkuu (CEO) wa kampuni ya Paypal nafasi aliyokuwa nayo kipindi hicho.

Mara ya pili alipojaribu kuchukua likizo alisafiri kwenye Afrika Kusini na Brazil, alipata malaria kali ambayo alinusurika kufa.

Na mara ya tatu alipochukua likizo, roketi ya kampuni yake ililipuka.

Kwa uzoefu huo, Elon alijiwekea sharti hilo kwamba hatachukua likizo kwenye kazi zake na hivyo amekuwa anafanya kazi kila siku, wakati

mwingine akilala kwenye viwanda vyake vya magari kuhakikisha uzalishaji unakuwa wa kiwango.

Na hilo limeweza kuwa na matokeo makubwa kwake.

## Magori; nje ya biashara sina mchezo mwingine.

John Magori, mwanamafanikio mwenzetu ambaye tuko naye kwenye KISIMA CHA MAARIFA tangu tumeanza mpaka sasa, huwa anatuma tathmini zake za kila mwezi zikiwa na ujumbe wenye nguvu mno, ambao nikiusoma huwa najiambia hakuna namna huyu mtu asifanikiwe. Nanukuu ujumbe huo kama ambavyo huwa anatuma;

*“Sababu kuu ya kupigania ndoto hii ni kwamba nje na biashara sina mchezo mwingine unaonipa burudiko na kuridhika, zaidi ya hilo naona dunia na jamii imenipa fursa na nyenzo zote muhimu kufanya kazi hii, zaidi sana bado kuna vingi vya kuboresha kwenye maeneo yote niliyochagua kufanyia kazi.” – John Magori*

Hebu soma tena sentensi hiyo, kwa John, biashara ndiyo mchezo wake, nje ya biashara hana kingine kinachompa burudani na kuridhika. Hii ina maana hakuna kitakachomrudisha nyuma na kila wakati atajihusisha na biashara.

Kwa sharti la aina hii, unaweza kuona wazi ni jinsi gani hawezi kuangushwa au kukatishwa tamaa na chochote, kwa sababu biashara ndiyo mchezo wake na nani asiyependa kucheza.

Sasa pata picha kuna mtu anataka kushindana naye, ambaye anaona huyu Magori anapata faida sana, wacha niige biashara yake, unafikiri mtu huyo ataweza kumshinda? Hilo halitawezekana, kwa sababu wakati yeye anaingia kushindana, mwenzake yuko kwenye mchezo.

## Makirita; nitaandika kila siku mpaka nakufa.

Tangu mwaka 2007 nimekuwa naandika, lakini kipindi cha mwanzo nilikuwa naandika pale ninapopata hamasa ya kuandika na hivyo

sikuwa naandika sana. Kati ya mwaka 2009 mpaka 2011 nilikuwa naandika zaidi kwenye mitandao ya kijamii, hasa Facebook.

Mwaka 2012 nilianza kuandika kwenye blog ambazo nilikuwa naanzisha, mwaka 2013 nikaanzisha blog ya AMKA MTANZANIA. Lakini bado sikuwa na mfumo mzuri wa kuandika, nilikuwa naweza nikaandika kwa wiki kadhaa, baadaye nikapotea na kuja kuandika tena baada ya miezi.

Mwaka 2014 nilianzisha KISIMA CHA MAARIFA na kuanza nidhamu ya kuandika kila wiki.

Tarehe 01/01/2015 nilijiwekea azimio la kuandika kila siku bila ya kuacha hata siku moja. Kama niko hai, hata kama mazingira yakoje, lazima niandike. Kuanzia tarehe hiyo mpaka leo ni siku 2202 ambazo nimeandika kila siku, bila kuacha hata siku moja. Na ushahidi ni makala za kurasa zilizopo kwenye mtandao wa KISIMA CHA MAARIFA.

Kwa sharti hili la kuandika kila siku nimeweza kuandika makala nyingi, chambuzi za kina za

zaidi ya vitabu 100 na vitabu zaidi ya 15. Yote hayo ni matokeo ya sharti nililojiwekea kwamba kila siku nitaandika na sijavunja sharti hilo.

Kuna kipindi nimekuwa kwenye mazingira magumu na ambayo ukiwa hujajiwekea sharti utajiambia leo siwezi kuandika, lakini mimi nina sharti, kila siku naandika, kama niko hai, nitaandika bila ya kujali niko kwenye mazingira gani au nini kinaendelea.

Ni sharti gani unakwenda kujiwekea kwenye maisha yako, sharti ambalo utalisimamia bila ya kulivunja hata kama kuna kila sababu inayokushawishi kuvunja?

Jiwekee sharti hilo sasa kulingana na mafanikio unayotaka kufikia na lifuate bila ya kulivunja.

## Hitimisho.

Rafiki yangu mpendwa, leo umeielewa kwa kina dhana ha ubatizo wa mafanikio.

Na umejua unapaswa kufanya ubatizo huo mwenyewe, kwa sababu hakuna atakayekufanyia kwenye jamii tuliyopo sasa.

Tenga muda na ufanye zoezi hili la ubatizo, kwa kuandika ndoto yako kubwa unayotaka kufikia, kisha kuandika kafara unazokwenda kutoa pamoja na masharti unayojipa.

Ni zoezi muhimu kufanya, lakini ni muhimu sana kuliishi.

Fanya zoezi hili na kwenye tafakari za mwezi nishirikishe kafara ulizochagua kutoa na masharti uliyojipa ili mara kwa mara niwe nakufuatilia kuona kama kweli unatekeleza hilo.

Najua umejitoa kweli kufanikiwa, hivyo hili unalipa uzito unaostahili.

Nikutakie kila la kheri na karibu tuendelee na safari hii pamoja.

## MAONI, SHUHUDA NA MASWALI.

Karibu kwa maoni, shuhuda na maswali kuhusu barua hii.

Kama kuna mahali hujaelewa na ungependa ufafanuzi zaidi basi karibu uulize swali.

Kama kuna eneo unaweza kuongeza maoni zaidi karibu pia.

Na kama una ushuhuda wa namna umewahi kufanyia kazi yale uliyojifunza kwenye barua hii, karibu utushirikishe matokeo ambayo uliyapata.

Maoni, maswali na shuhuda viwekwe moja kwa moja kwenye kundi la KISIMA CHA MAARIFA wasap.

Nikutakie kila la kheri katika kufanyia kazi haya uliyojifunza kwenye barua hii.

Rafiki yako anayekupenda sana,

Kocha Dr. Makirita Amani,

www.amkamtanzania.com/kocha

0755 953 887 / kochamakirita@gmail.com

**MUHIMU;** KAMA HUJAPATA BARUA ZA NYUMA, FUNGUA; www.kisimachamaarifa.co.tz/barua2021